www.repoa.or.tz

Toleo Na 1/2021 Machi 2021

Dokezo la Utafiti

# Uwiano Kati ya Aina ya Kazi, Taarifa Kuhusu Kazi, Stadi za Kazi, na Elimu

Na Paschal B. Mihyo, Donald E. Mmari na Jamal B. Msami

Kwenye dokezo hili tunanatoa muhstasari mfupi wa sura mbali mbali zilizopo kwenye kitabu kiitwacho 'Youth Transition from School to Work: A Case Study of VETA in Tanzania (Kipindi cha Mpito kwa Vijana Kati ya Mafunzo na Ajira: Mchango wa VETA Tanzania), chenye lengo la kuongeza uelewa wa matatizo wanayopitia vijana kwenye jitihada zao za kutafuta ajira baada ya mafunzo. Nia ni kutafuta njia ya kuwapunguzia vikwazo hivyo na kuongeza mchango wao kwenye jitihada za taifa za kujenga uchumi unaoongozwa na Viwanda. . Kwenye dokezo hili tunaangalia mambo gani yanawasaidia au kuwapunguzia vijana uwezo wa kupata ajira mara tu baada ya mafunzo, hasa kuhusu jinsi wanavyotayarishwa kuingia kwenye ulimwengu wa kazi, matarajio yao ukiyalinganisha na hali halisi kwenye soko la ajira na uhusiano ulioko kati ya kazi zilizopo, taarifa kusu hizo kazi, stadi wanazokuwa nazo na viwango vyao vya elimu.

## VIDOKEZO MUHIMU

- Elimu ni ufunguo wa kuwaongezea vijana uwezo wa kujifunza, kupata ajira za muda mrefu na kuongeza tija na ufanisi katika kazi zao hasa kama itawapa ujuzi na stadi zinazolingana na uwezo unaotakiwa kwenye fani mbali mbali katika maeneo ya kazi kulingana na mabadiliko ya haraka yanayojitokeza katika nyanja hizo.
- Uelewa wa kutosha juu ya hali halisi kuhusu mazingira ya soko la ajira ni muhimu katika kuwatayarisha vijana juu ya matumaini yao na kupunguza muda wa kutafuta kazi baada ya kuhitimu masomo yao.
- Elimu ya ufundi ni muhimu kwa kuwajengea vijana stadi  na inaweza kuwasaidia vjina kupata ajira haraka kama stadi hizo zimejikita kwenye matarajio ya waajiri kwenye sekta za viwanda na huduma.
- Mafunzo yakizingatia mchanganyiko sahihi wa ujuzi, nadharia na ufundi na kutoa stadi zinazohitajika kwenye nyanja nyingi za uzalishaji na matakwa mahsusi ya maeneo husika, yataongeza uwezekano wa vijana kupata ajira haraka baada ya mafunzo.

## Utangulizi na Madhumuni

Inakadiriwa kwamba kila mwaka ni kati ya vijana 50,000 na 60,000 tu miongoni mwa vijana milioni moja wanaongia kwenye soko la ajira kila mwaka ambao hubahatika kupata ajira kwenye sekta rasmi. Hivyo wengi wao, zaidi ya vijana 900,000 hujaribu kujiajiri au huingia kwenye sekta isiyo rasmi au huendelea kutafuta ajira. Wanaoingia kwenye sekta isiyo rasmi hupata ajira fupi zenye kipato kisochoaminika na kisichokidhi mahitaji yao. Ajira zao huwa kwenye mazingira duni ya kazi yasiyo na mikataba, mapato ya kutosha, bima ya afya au kinga dhidi ya ukosefu wa kipato. Kipindi cha mpito kwenye kitabu hiki kinahusu muda unaoutumiwa na vijana kati ya kuhitimu mafunzo na kupata ajira yenye mkataba na yenye mazingira bora ya kazi (ILO 2018). Utafiti wa Shirika la Kazi Duniani uliofanywa Tanzania (2013) unaonyesha kwamba vijana hutumia wastani wa miezi 19.4 wakitafuta ajira na wastani wa  miezi 21 bila ajira. Wengine humaliza wastani wa miezi 37.7 wakiwa wamejiajiri. Kitabu hiki kinaangalia mchango wa VETA kwenye kuwaongezea vijana uwezekano wa kuajiriwa baada ya kuhitimu masomo yao.

## Mbinu za Utafiti zilizotumiwa

Utafiti huu ulitumia mchanganyiko wa mbinu mbali mbali za kupima taarifa za wingi na ubora wa takwimu husika. Tuliwahoji watu 574 —kati yao wakiwemo wahitimu wa VETA 210, wanafunzi wa VETA 210, walimu 105 na waajiri 49. Wahojiwa walichaguliwa kutumia vigezo maalum kutoka halmashauri mbali mbabli zenye vituo vya VETA zikiwemo halmashauri za Jiji la Arusha, Jiji la Dodoma, Manispaa Ilala, Manispaa ya Ilemela, Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa, Manispaa ya Kinondoni, Manispaa ya Lindi, Manispaa ya Mbeya, Manispaa ya Morogoro, Manispaa ya Temeke, na Manispaa ya Ubungo.

## Matokeo ya utafiti kuhusu sababu zinazoongeza au kupunguza muda wa mpito kwa vijana

### *Uhusiano kati ya muda wa masomo, matarajio ya wahitimu na urefu wa muda wa mpito*

Masomo yakichukua muda mrefu yakafuatiwa na kipindi kirefu cha wahitimu kutafuta ajira, kunakuwa na hisia mbaya kwenye jamii na miongoni mwa wahitimu kuhusu manufaaa ya elimu. Hisia hizi zinakuwa mbaya zaidi ikiwa waliohitimu mafunzo ya shule za msingi au sekodari wanafanikiwa kupata ajira kwa haraka zaidi kuliko wahitimu wa elimu ya juu. Tafiti kuhusu nchi mbali mbali zinaonyesha kwamba kuna idadi kubwa ya wasiokuwa na ajira miongoni mwa wahitimu wa elimu ya sekondari kuliko wale wenye elimu ya msingi na pia wenye elimu ya sekondari wanapata ajira kwa urahisi kuliko waliofuzu elimu ya juu. Aidha wale ambao hawakupata elimu rasmi wanapata ajira kwa urahisi zaidi ya walio na elimu[1]. Utafiti pia unaonyesha tatizo hili linatokana na jinsi vyuo vikuu vinavyowajengea wanafunzi matumaini ya hali ya maisha baada ya kuhitimu yasiyoendana na hali halisi kwenye jamii na jinsi mafunzo ya ufundi na stadi yanavyowatayarisha vijana vizuri zaidi kwa maisha na mazingira ya kazi.[2] Inaonekana kwamba mfumo wa elimu usioendana na hali halisi ya maisha kwenye jamii inawatayarisha wahitimu kupata mshtuko kisaikolojia na kuwasukuma kuendelea kutafuta kazi zenye vipato na hali ya maisha ya juu ambazo ni chache na zinahitaji uwezo na uzoefu ambao bado hawana. Hii inaongeza kipindi cha mpito kwa wengi wao.

### *Matayarisho finyu na ujuzi mdogo*

Mwaka 2016, Kelvin Balogoun, Rais wa Coca-Cola ukanda wa Afrika ya Kati, Mashariki na Magaharibi, alisema kwamba takriban milioni tano kati ya wahitimu milioni kumi wa vyuo vikuu 668 barani Afrika, hawapati ajira kwa sababu hawapati ujuzi wa kutosha na wachache wanaoajiriwa na Coca-Cola hupewa mafunzo kazini.[3] Hii ina maana wengi wa wahitimu hawapati ujuzi wa kutosha. Pai Obanya pia ametoa wazo kwamba kuna tofauti kati ya kwenda shule na kuelimika kwa sababu mtu anaweza akapita kwenye mfumo wa elimu na kupata elimu ambayo inamuacha akijua yale alivyojifunza lakini hayakumpa ujuzi wa kutosha.[4]

Tatifi nyingi zimeonyesha kwamba licha ya vipindi virefu vya mafunzo, wahitimu ambao hawajatayarishwa kukubalika kwenye mazingira ya kazi ya wakati huo, hupitia vipindi virefu vya kutafuta ajira.

### *Uelewa wa vijana kuhusu hali ya soko la ajira*

Wahitimu ambao humaliza mafunzo wakiwa na matumaini makubwa ya kupata ajira haraka, hujikuta wamekata tamaa pale matarajio yao hayafikiwi kwa haraka na ni rahisi vijana waliokata tamaa kuacha kabisa kutafuta ajira na kuwa katika kundi la wasio na shughuli maalum.[5] Pia kwenye jamii mbali mbali utamaduni unachangia kwenye tatizo la kukosa ajira. Kwenye baadhi ya jamii vijana wa kiume wakibalehe hutarajiwa kuondoka na kwenda nje ya jamii kutafuta ajira au mali. Hawatarajiwi kutafuta ajira au shughuli kwenye jamii zao na huwafanya waende kwenye maeneo ambayo tayari yana uhaba wa ajira. Matokeo ni kwamba huwa wanachukua muda mrefu kabla ya kupata ajira. Utafiti umeonyesha kwamba mfumo wa elimu rasmi na utamaduni kwenye jamii vinachangia kwenye kujenga matumaini ya vijana kuhusu maisha baada ya mafunzo. Ushiriki wa jamii katika kushauri vijana unaweza kuwaandaa kujishughulisha katika jamii baada ya kuhitimu masomo.

## Hitimisho na Mapendekezo

Utafiti umeonyesha kwamba kuna mambo manne yanayochelewesha au kuharakisha vijana kupata ajira katika kipindi cha mpito kutoka kwenye mafunzo hadi kuajiriwa: aina ya kazi, taarifa kuhusu kazi, stadi za kazi, na elimu wanayopewa (Angalia kilelezo na 1).

---

[1] Loprest, P., Spaulding, S. and Nightingale, D. S. (2019), 'Disconnected Young Adults: Increasing Engagement and Opportunity', RSF: The Russell Sage Foundation *Journal of the Social Sciences, 5(5), pp. 221.*

[2] Dockery, A, 2010, Education and happiness in the school to work transition, National Centre for Vocational Education Research, Adelaide, , Australia. Available at: https://files.eric.gov/fulltext/ED509308.pdf (Accessed on 23-03-2019)

[3] ACET, 2016, Unemployment in Africa. No jobs for 50% graduates, Available at: https://www.acetforafrica.org (Accessed on 23-03-2019)

[4] Obanya, P.A.J, 2006, Education as An Integral Aspect of Africa's Evolutionary Process, Quality of Human Resources Education, Vol. II, Encyclopaedia of Life Support Systems.

[5] Dvouletý, O., Mühlböck, M., Warmuth, J. and Kittel, B. 2018, ''Scarred' young entrepreneurs. Exploring young adults' transition from former unemployment to self-employment', *Journal of Youth Studies, 21(9), pp. 1159-1181.*

**Aina ya kazi** inatokana na ajira zinazotakiwa kwenye viwanda na sekta zingine. Kama kazi husika hazihitaji ujuzi wa ngazi ya kati au ya juu watu wenye ujuzi na ufundi wa kati au wa juu hawawezi kupata ajira kwa muda mfupi. Pia kama hazihitaji ujuzi na teknolojia ya kisasa, walioenda mbali kwenye elimu hawawezi kupata ajira kwa urahisi.

***Pendekezo:*** Wawekezaji wahimizwe kuwekeza kwenye shughuli zenye tija na zenye uwezo wa kutumia stadi za kisasa ili kuongeza uwezekano wa vijana wenye elimu na stadi husika kuajiriwa.

**Taarifa kuhusu ajira** zina umuhimu sana kwenye kusaidia vijana kupata ajira. Umuhimu wa kwanza ni taarifa kuhusu mafunzo na stadi zinazotolewa na VETA. Vijana wengi vijijini na sehemu za pembezoni mijini hawapati taarifa hizi. Umuhimu wa pili ni kuhusu taarifa za ajira ambazo haziwafikii wale walio kwenye maeneo yenye matatizo ya mitandao au yasiyo unganishwa na taarifa hizo.Tatu ni matumizi ya tehama kwenye mafunzo ya ufundi na elimu kwa ujumla ambayo utafiti unaonyesha kuwa hayatumiwi kwa kiwango sahihi.

***Pendekezo:*** Jitihada ziongezwe kwenye kujenga uwezo wa vijana wengi kupata taarifa za mafunzo na elimu hasa vijijini na sehemu za pembezoni wa miji. Pia VETA iongezewe uwezo wa kutumia tehama kwenye mafunzo ya ufundi na ustadi.

**Ujuzi** unaojengwa na VETA unaonekana kuwa wa kawaida na kuna stadi muhimu kwa kazi ambazo zinaambatana na maadili na nidhamu kazini ambazo bado hazitiliwi mkazo. Pia stadi zinazoweza kuwasaidia vijana kupata ajira sehemu za vijijini hazipewi uzito upasao. Mbali na hayo kuna umuhimu wa VETA kuangalia ujuzi gani utahitajika kwenye miaka michache ijayo ili kuwatayarisha vijana kupata ajira.

***Pendekezo:*** Kuna umuhimu wa VETA kufanya tathmini yakinifu kuhusu mahitaji ya wawekezaji na wazalishaji sehemu za mijini na vijijini na hasa vijijini kwa sababu ajira nyingi ziko kwenye maeneo ya vijijini hususani kwenye kilimo, mifugo, misitu, uvuvi, ufugaji wa nyuki na mengine. Pia VETA iwezeshwe kutoa stadi zenye mvuto zaidi kutokana na mafunzo ya vitendo zaidi ya nadharia na kuwapeleka wanafunzi kwenye maeneo ya kazi kwa mazoezi wapate uzoefu.

**Elimu** inakubalika kuwa ni ufunguo wa maisha. Hata hivyo, utafiti umeonyesha kwamba kwenda shule na kuelimika siyo kitu kimoja kwa sababu shule inaweza kumpa mtu elimu bila kumpa ujuzi na stadi za kuendeleza maisha au jamii yake. Ni dhahiri kutokana na hilo kwamba ili elimu kuwa msaada lazima ijenge wahitimu wenye ufahamu kuhusu mahitaji ya jamii zao na uwezo wa kujiendeleza wao na jamii zao. Utafiti wetu umeonyesha kwamba vyuo vya VETA vinangalia zaidi maendeleo ya mwanafunzi bila kuyaunganisha na maendeleo ya jamii. Stadi na maarifa ambayo ni muhimu kumwendeleza mtu kimaisha na kumsaidia kutumia kikamilifu ujuzi wa kiufundi hazipewi kipaumbele sana.

***Pendekezo:*** Vyombo vinavyosimamia mafunzo vijiongezee uelewa wa mahitaji ya sekta mbali mbali na viwe na mifumo ya kuviwezesha vyo vya ufundi kuangalia mahitaji ya sekta hizo kwa sasa na baadaye ili kuwasaidia wahitimu wake kuingia na kukubalika kwa haraka na kwa urahisi kwenye mifumo ya ajira.

### Kielelezo 1: Uwiano kati ya aina ya kazi, taarifa kuhusu masomo na kazi, ujuzi na elimu



REPOA
157 Mgombani/REPOA Street, Regent Estate
P.O. Box 33223, Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +255 22 2700083, Cell: +255 75 409 1677 Fax +255 22 2705738
Website: www.repoa.or.tz Email: repoa@repoa.or.tz

Kituo cha Taarifa na Maarifa, REPOA
Kituo chetu cha Taarifa na Maarifa kinatoa mazingira mazuri kwa utafiti wa fasihi na vitabu/ maandiko mbali mbali kwa haraka na kwa urahisi wa matumizi ya maarifa na taarifa. Imeunganishwa na wavuti (internet) kwa ajili ya matumizi ya maktaba ya mkondoni (online) kuwasaidia wanaosomea Shahada za Uzamili na Uzamivu, watafiti na wasomi kwa kuwapatia magazeti, vitabu, ripoti n.k. ya siku za karibuni.

Saa za Ufunguzi
Kituo cha Taarifa na Maarifa kinakuwa wazi kuanzia Jumanne hadi Ijumaa saa 4.00 asubuhi hadi saa 7.00 mchana, saa 8.00 mchana hadi saa 11.00 alasiri. Maktaba ya mkondoni (online) ni wazi saa 24 kila siku.

@REPOA 2021
Matokeo, tafsiri, hitimisho, na maoni yaliyotolewa humu ndani ni ya mwandishi na siyo lazima yawe yanaakisi maoni na sera za REPOA.